CARDINAL RUGAMBWA
MEMORIAL UNIVERSITY COLLEGE
A Constituent College of the Saint Augustine University of Tanzania

Website: www.carumuco.ac.tz | Email: info@carumuco.ac.tz | Mob: +255 782 323923, +255 763 310446

FAHAMU MAANA NA UMUHIMU WA ISIMU YA LUGHA (LINGUISTICS)

Je, umewahi kujiuliza ni ala (organ) zipi zinahusika kutamka sauti fulani? Sauti ni kitamkwa ambacho huoneshwa kwa alama ya umbo fulani, mfano /b/, /p/, /m/ n.k. Nini basi kinafanyika kuvitofautisha vitamkwa au sauti mbili zinazotamkiwa sehemu moja, kwa mfano /b/ na /p/? Je,umewahi kujiuliza kwa nini watu wengine, kama bubu, hawawezi kuongea? Kwa nini neno moja katika lugha fulani lina maana nyingi na halileti utata? Kwa nini watu wengine hawezi kuitamka sauti fulani? Kwa mfano, Wahaya huwawia vigumu kutamka sauti ng' /ŋ/ katika maneno kama vile ng'ombe,ng'ang'ana; Wakurya /l/katika neno kula; Wasukuma /r/ katika neno kura, kwa kutaja baadhi. Je uhusiano wa lugha na jamii ni upi ?Maswali hayo na mengine mengi ndio huwafanya wanaisimu (linguists) kushughulika kila kuchapo kwa kufanya tafiti mbalimbali ili kutafuta majibu ya maswali hayo.

Sasa, nini maana ya isimu (linguistics)? Isimu yaani *linguistics* ni sayansi ya lugha. Taaluma hii, huichambua lugha na kutafiti jinsi mfumo wa sauti unavyofanya kazi. Hata hivyo, baadhi ya watu wana fikra potofu kuhusu dhana ya linguistics. Baadhi ya dhana potofu zinazohusu istilahi *linguistics* ni kama vile:

(a).Linguistics ni somo la Kiingereza. Pengine fikra hiyo inatokana na sababu kwamba neno hilo ni la lugha ya Kiingereza. Je, tunapotumia kisawe chake cha Kiswahili yaani 'Isimu' bado maana inabaki kama ilivyo katika lugha ya Kiingereza yaani *linguistics*? Bila shaka, maana yake ni ile ile. Kumbe linguistics siyo Kiingereza, isipokuwa kuna Isimu ya Kiingereza (English Linguistics), Isimu ya Kiswahili (Swahili Linguistics) n.k. Mwenye kujifunza taaluma hii, anaweza kujikita katika somo moja tu au kujikita katika uchambuzi wa lugha kwa ujumla. Mtaalamu wa Isimu anaweza kuchambua lugha yoyote duniani kwa kutumia kanuni za sayansi ya lugha.

(b). Linguistics ni kujua lugha nyingi. Hii pia ni dhana potofu. Wengi hufikiri anayesoma linguistics anafahamu kuongea na kuandika lugha nyingi. Mwenye kujua lugha nyingi (kuongea na kuandika) ni mjuvi wa lugha nyingi yaani (multilingual) kama ilivyo kwa mwenye kujua lugha mbili anavyofahamika kama mjuvi wa lugha mbili (bilingual). Kufahamu lugha nyingi, kuziongea na kuziandika, hakumaanishi mtu huyo anaweza kuzichambua lugha hizo. Kwa mfano, Watanzania wengi ni wamilisi wa lugha ya Kiswahili. Mathalani, mtu fulani akisema 'mtoto changu' au 'kiatu zangu' hata mtoto mdogo atamkosoa na kumwambia hatusemi hivyo! Bali 'mtoto wangu' au 'kiatu changu'. Lakini kueleza kwa nini mzungumzaji atumie umbo wa- badala ya umbo cha- katika tungo 'mtoto changu' na umbo cha- badala ya umbo za- katika tungo 'kiatu zangu', si jambo rahisi na pengine hataweza kabisa kufanya hivyo.

(c). Wengine hudhani linguisticsni ni kufahamu Kiingereza vizuri. Utasikia watu wengi wakiwaambia wenzao kwa vile unasoma au umesoma linguistics, basi wewe ni mahiri wa lugha ya Kiingereza au uko vizuri sana katika lugha ya Kiingereza. Swali la msingi tunalopaswa kujiuliza, je nchi zisizotumia Kiingereza somo la linguistics halipo? Sasa basi, linguistics ni nini? Kama tulivyoeleza hapo juu, linguistics ni sayansi ya lugha kwa sababu taaluma hii huichunguza lugha kisayansi kwanza kwa kuangalia mfumo wa sauti, mwelekeo wa mkondo-hewa na hadi kupata maumbo kama /a/ /b/ /p/ /d/ /t/ n. k. Aidha, isimu huchunguza jinsi ambavyo sauti huunda maneno, na maneno kuunda sentensi, namna gani mtoto hujifunza lugha. Fauka ya hayo, isimu huchunguza maana ya maana na aina za maana. Hivyo isimu huhusika na mambo mengi yahusuyo lugha.

Taaluma ya isimu inayo matawi mbalimbali kama vile:

(i) Isimu saikolojia (psycholinguistics)

Ni tawi la isimu ambalo huchunguza namna ambavyo mtoto hupata lugha toka hatua za awali, na jinsi mtu mzima anavyojifunza lugha nyingine tofauti na ya kwanza pamoja na uhusiano wa lugha na ubongo. Nini kinachomwezesha mtoto kujua lugha? Kimsingi binadamu hazaliwi na lugha. Kwanini mtu mzima hupata shida kujifunza sauti mpya ambazo hakuzizoea?

(ii) Isimu jamii (Sociolinguistics) tawi la isimu ambalo hujihusisha na uchunguzi wa uhusiano uliopo baina ya lugha na jamii.

Matawi mengine ya isimu nikama vile lugha na kompyuta (artificial intelligence), Isimu historia na isimu linganishi (historical & comparative linguistics),Isimu ubongo na isimu neva (cognitive linguistics and neurolinguistics) n. k.

Mbali na matawi, linguistics (Isimu) ina viwango vya lugha (levels) mbalimbali ambavyo hushughulika navyo kama:-

Pragmatiki (pragmatics)- ni taaluma inayojishughulisha na maana ya maneno kulingana na muktadha wa wahusika na jamii husika. Neno fulani laweza kuwa na maana chanya katika jamii moja na kuwa na maana hasi katika jamii nyingine.

Fonetiki (phonetics)- taaluma inayohusu mfumo wa sauti za lugha ya binadamu, katika kuzitamka (fonetiki matamshi - articulatory phonetics), kuzisikia (fonetiki masikizi - auditory phonetics) na kuzielewa (fonetiki akustika - acoustic phonetics).

Semantiki (semantics) – kiwango hiki cha lugha hujishughulisha naa maana katika lugha. Mofimu, neno na sentensi zinavyojenga maana katikaa lugha.

Sintaksia (syntax) – mpangilio wa maneno katika sentesi kulingana na kanuni za lugha husika (sarufi ya lugha)

Mofolojia (morphology) - muundo na mpangilio wa mofimu katika neno na jinsi maneno yanavyoundwa katika lugha.

HISTORIA YA ISIMU (LINGUISTICS) KWA UFUPI

Isimu kama taaluma inayojitegemea ilianza karne ya 19. Hata hivyo wanafalsafa walianza kujishughulisha na masuala ya lugha tangu zamani kama karne ya 5-3 KK hasa kwa kukitalii kipengele cha maana. Wataalamu wa mwanzo walianza kuchambua lugha za Kigriki na Kilatini. Lugha hizo ndizo ziliaminiwa kuwa na sarufi bora na hivyo kutumika kama kiunzi cha kupimia sarufi nyingine mpaka karne ya 19, na nusu ya kwanza ya karne ya 20 walipotokea wataalamu kama Ferdinand de Saussure, Bloomfieldambao waliitazama lugha kwa kuangalia mfumo wa sarufi na baadaye Noam Chomsky aliyeibua mfumo wa sarufi zalishi.

Kadri wataalamu wanavyoendelea kutafiti na kuvumbua, imegundulika kuwa isimu ni sayansi ya ajabu ambayo inajihusisha na kitengo cha lugha ya binadamu (human language faculty) na jinsi kitengo hicho kinavyofanya kazi katika kuifahamu na kujifunza lugha. Vile vile isimu ina uhusiano mkubwa na sayansi nyingine kama fizikia (fonetiki masikizi na fonetiki akustika - auditory and acoustic phonetics), biolojia (isimu ubongo - cognitive and neurolinguistics), sayansi ya kompyuta(computer science artificial intelligence), saikolojia (isimu saikolojia - psycholinguistics) falsafa (semantiki) n. k.

ISIMU KATIKA CHUO KIKUU KISHIRIKISHI CHA SAUT CHA KUMBUKUMBU YA KARDINALI RUGAMBWA (CARUMUCO)

Chuo hiki kilichopo Bukoba maeneo ya Nkindo kata ya Karabagaine, kinatoa Astashahada (certificates), Stashahada (Diploma) mbalimbali, Shahada ya Sanaa na Elimu na Shahada ya Umahiri katika Elimu. Linguistics ni moja ya masomo yanayosomwa na wanachuo wa Shahada ya Sanaa na Elimu, wenye upendeleo wa kufahamu na kufundisha lugha.

Idara ya isimu na lugha inao wataalamu, vifaa na mazingira mazuri ya kujifunza somo hilo. Wanachuo wa CARUMUCO wanaosoma Linguistics, huwa wataalamu, wachambuzi na watafiti wanaojiamini katika masuala ya sayansi ya lugha.Chuo kina maabara ya kompyuta. Wanachuo wanaosoma isimu huitumia kujifunza matamshi ya sauti mbalimbali.

Je, isimu (linguistics) ina umuhimu gani?

Isimu ina umuhimu mkubwa katika kumwezesha mwanadamu, hasa mhitimu wa taaluma ya isimu, kushughulika na masuala ya lugha. Kwanza kabisa, mtu mwenye maarifa ya isimu huwa mwepesi katika kujifunza lugha yoyote kwa sababu amejifunza matamshi ya sauti za lugha kwa ujumla.

Vile vile humwezesha mtu kufanya uchambuzi wa lugha na kujifunza kanuni za lugha nyingine kwa urahisi. Anakuwa pia na uwezo wa kufahamu kwanini watu fulani hawawezi kutamka sauti fulani na wengine wanaweza. Mtu mwenye maarifa ya isimu hapati mshangao kwanini watu fulani hutamka hivi na wengine vile.

Uwezo wakufundisha lugha. Mtu mwenye maarifa ya linguistics, anaweza kuwa mwalimu mzuri wa lugha yoyote ambayo atapenda kuwa mahiri kwayo.

Si hivyo tu, bali mwanaisimu (linguist) huweza kufanya tafiti mbalimbali katika sayansi ya lugha zikiwemo za kuelewa nafasi ya lugha katika ubongo.

Zaidi ya yote mtaalamu wa linguistics anaweza kutoa tiba matamshi kwa mtu mwenye matatizo ya kuongea hasa kwa wale wanaopoteza lugha au sauti fulani fulani kutokana na majanga mbalimbbali mfano ajali zinazoweza kuumiza sehemu ya lugha kwenye ubongo (speech impairment). Hizo ni baadhi ya faida/ umuhimu wa kusoma *linguistics*.

Sanjari na utoaji wa maarifa ya kujifunza uchambuzi wa lugha kisayansi, CARUMUCO pia inatoa maarifa ya kujifunza lugha ya Kiingereza kwa wanachuo wote, ambapo kila mwanachuo bila kujali kozi na fani anayosomea hupaswa pia kusoma kozi ya Kiingereza ijulikanayo kama Practical English. Kozi hii huwawezesha wanachuo wa CARUMUCO kuongeza ujuzi wa Kiingereza, kukifahamu vema hasa kukiongea na kukiandika vizuri kwa kuzingatia sarufi ya lugha (Grammar).

Njoo CARUMUCO upate ujuzi, njoo CARUMUCO upate mbinu za kuwa mtafiti na mtaalamu katika masuala mbalimbali kwa maendeleo endelevu.

Sr. Josephiter Joseph
Idara ya Isimu na Lugha (Departiment of Linguistics and Languages),

Karibu! CARUMUCO

"Higher Education for Sustainable Development!"

Pia tunatoa programu mbalimbali katika nyanja zifuatazo:-

Postgraduate Programmes
i. Master of Education Management
Undergraduate Programme
ii. Bachelor of Arts with Education
Diploma Programmes
i. Diploma in Education
ii. Diploma in Primary Education
iii. Diploma in Law
iv. Diploma in Accounts and Finance
v. Diploma in Procurement and Supply chain management
vi. Diploma in Information Technology
Certificate Programmes
i. Certificate in Law
ii. Certificate in Accounts and Finance
iii. Certificate in Procurement and Supply chain management
vi. Certificate in Information Technology